BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 24 Mei, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI YA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ustawi wa Jamii:

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2017/2018.

III. MASWALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

64. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa baada ya Serikali kusaini Mkataba wa Ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Amali Daya Mtambwe, shughuli hiyo ya ujenzi ilianza kwa kung'oa mikarafuu mingi katika eneo hilo jambo ambalo ni hasara ukizingatia kwamba Mtambwe kuna maeneo mengi ya ardhi nzuri za kujenga Chuo hicho bila ya kung'oa mikarafuu.

(a) Je, ni sababu gani hasa zilizopelekea Serikali kuacha maeneo yaliyokuwa hayana mikarafuu, na kuamua kung'oa mikarafuu kwa ajili ya ujenzi huo.

(b) kwa kuwa ujenzi huo ulisita kwa muda mrefu. Je, ni lini ujenzi huo utaanza na lini utamalizika ili Chuo hicho kianze kutumika.

(c) Je, ni sababu gani hasa zilizomfanya Mkandarasi asimamishe ujenzi huo.

Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

164. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi sana katika kuleta maendeleo ya Zanzibar na wananchi wake hasa vijana. Katika maendeleo hayo ni pamoja na Zanzibar kupata fursa ya kitaifa na kimataifa ili vijana wetu wapate manufaa ya ajira na sifa ya nchi yetu. Moja ni hili la kupata nafasi ya kushiriki mashindano ya CAF.

(a) Je, Serikali inafahamu kwa kina tabu tulizozipata mpaka kufanikiwa. Kama inafahamu kwanini tunaachia watu wachache kwa manufaa yao watuharibie sifa zetu.

(b) Je, Serikali imejipanga kwa mipango madhubuti ya kifedha, dawati la ufundi, na mengineyo au tunasubiri lala salama.

(c) Je, Serikali imejitayarishaje kwa hapa tulipofika na hatua za baadae.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

35. MHESHIMIWA SHAIBU SAID ALI (Jimbo la Chonga) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Hivi sasa kuna ongezeko kubwa la watoto mayatima katika visiwa vya Unguja na Pemba, suala ambalo litapelekea watoto hao kuwa watoto wa mitaani, wizi, wala unga na kadhalika kutokana na watoto hao kukosa huduma kamili za kijamii.

(a) Je, kuna utaratibu gani wa kuwachukuwa watoto hao na kuwapeleka kwenye nyumba za kulelea watoto.

(b) Je, Serikali kuwaachia watoto hawa kuzurura ovyo, haioni itapelekea kuongezeka kwa kundi la wavuta unga, wezi, wazururaji hapo baadae.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

66. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Zanzibar inakabiliwa na kipindi kirefu cha kiangazi hali iliyosababishwa na mabadiliko ya Tabia Nchi sambamba na uharibifu wa mazingira. Hali hii imesababisha baadhi ya mito kukauka muda mfupi tu baada ya msimu wa masika kumalizika na kusababisha upungufu mkubwa wa maji kwenye maeneo ya kilimo na kadhalika.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyadhibiti maji ya mvua ili kubaki muda mrefu kwenye mito ili yaweze kutumika wakati wa kiangazi badala ya kuachwa maji hayo kuingia baharini kama ilivyo hivi sasa.

(b) Je, Serikali kupitia Wizara yako ina mpango gani wa makusudi wa kuirudishia mito uhalisia wake wa kuhifadhi maji kwa muda mrefu kwa kupanda miti kando kando ya mito kama vile mitomondo, mikangachale, misamaka, michekechu, miwale na mibie.

(c) Je, Serikali haioni kwamba kwa sasa ipo haja ya kuanzisha utaratibu wa kuitunza na kuihifadhi miti ya asili kama wanavyotunza wahifadhi wa misitu ya asili.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko

27. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Wizara imekuwa ikihamasisha uanzishwaji wa viwanda vidogo vidogo na viwanda hivyo vimeanzishwa katika maeneo mbali mbali yanayoishi wananchi.

(a) Je, Wizara inatambua mpaka sasa ina viwanda vidogo vidogo vingapi Unguja na Pemba.

(b) Je, viwanda hivyo vinafanyiwa ukaguzi wa viwango na ZBS.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

139. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Chukwani) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kwa kuwa maeneo mengi ya vijijini yamekuwa na changamoto ya nyumba za wafanyakazi hasa madaktari na walimu na baadhi ya maeneo haya kuna nyumba ambazo zinahitaji matengenezo au ukarabati.

Je, ni sababu gani zinazosababisha nyumba hizi zisifanyiwe ukarabati ili wafanyakazi mbali mbali waweze kuishi katika nyumba hizo na kuwaondoshea usumbufu.

144. MHESHIMIWA DKT. MWINYIHAJI MAKAME MWADINI (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kumekuwa na msongamano mkubwa wa gari katika eneo la Malindi hasa nyakati za mchana.

(a) Je, Wizara imefanya utafiti wa kina kujua nini tatizo la msongomano huo.

(b) Je, baada ya utafiti huo, hatua gani Wizara imechukuwa kuidhibiti hali hiyo.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

110. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Pamoja na jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuondoa kabisa tatizo la maji Zanzibar, vyanzo vya maji vimepunguza utoaji wa maji na hivyo kuwepo tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama. Nchi nyengine hutumia hata maji ya chumvi kwa kuyabadilisha kuwa ya kawaida na kuweza kutumika kwa matumizi mbali mbali.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kuhakikisha kuwa inayahifadhi maji ambayo wakati wa mvua hujaa katika bwawa kubwa la Mwanakwerekwe ili maji hayo yasipotee bure.

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kulitafutia ufumbuzi bwawa hilo ambalo pengine ni kama hidaya kwetu kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

(c) Ni utafiti gani umefanywa kuona kwamba maji hayo yanaweza au hayawezi kutumika kwa matumizi ya binaadamu.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa Mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
24 Mei, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.